*Yohana 1:1, 3-5, 9-10, 14 (NENO)*

# Neno alikuwa Mungu… Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima na huo uzima ulikuwa nuru ya watu… Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu

---

**Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. … Vitu vyote viliumbwa kwa yeye, wala pasipo yeye hakuna chochote kilichoumbwa ambacho kimeumbwa. Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima na huo uzima ulikuwa nuru ya watu. Nuru hung’aa gizani nalo giza halikuishinda. … Kwamba nuru halisi, imwangaziayo kila mtu ilikuwa inakuja ulimwenguni. Huyo Neno alikuwako ulimwenguni na ingawa ulimwengu uliumbwa kupitia kwake, haukumtambua. … Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu, nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba, amejaa neema na kweli.**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yohana 3:18-21 (NENO)*

# Watu wakapenda giza kuliko nuru... yule aishiye kwa ukweli huja kwenye nuru



Yeyote amwaminiye hahukumiwi, lakini asiyeamini amekwisha kuhukumiwa, kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu. Hii ndiyo hukumu kwamba: Nuru imekuja ulimwenguni, nao watu wakapenda giza kuliko nuru kwa sababu matendo yao ni maovu. Kwa kuwa kila atendaye maovu huchukia nuru, wala haji kwenye nuru ili matendo yake maovu yasifichuliwe. Lakini yule aishiye kwa ukweli huja kwenye nuru, ili ionekane wazi kwamba matendo yake yametendeka katika Mungu."

*Spiritual Warfare Cards.com*

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yohana 8:12, 24, 31-32, 34, 36 (NENO)*

# Kama mkidumu katika maneno yangu... kweli itawaweka huru... kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi... Mwana akiwaweka huru mtakuwa huru kweli kweli



---

**Kisha Yesu akasema nao tena akawaambia, "Mimi ni nuru ya ulimwengu. Mtu yeyote akinifuata hatatembea gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima." ... Niliwaambia kuwa mtakufa katika dhambi zenu, kwa maana msipoamini ya kwamba 'Mimi Ndiye,' mtakufa katika dhambi zenu." ... Kisha Yesu akawaambia wale Wayahudi waliomwamini, "Kama mkidumu katika maneno yangu, mtakuwa wanafunzi wangu kweli kweli. Ndipo mtaijua kweli nayo kweli itawaweka huru." ... Yesu akajibu, "Amin, amin nawaambia, kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi. ... Hivyo Mwana akiwaweka huru mtakuwa huru kweli kweli.**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yohana 15:7, 9, 11-14, 16 (NENO)*

# Furaha yangu iwe ndani yenu... Mpendane kama mimi nilivyowapenda ninyi... mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake



Ninyi mkikaa ndani yangu na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni lolote mtakalo, nanyi mtatendewa. ... “Kama vile Baba alivyonipenda mimi, hivyo ndivyo mimi nilivyowapenda ninyi. Basi kaeni katika pendo langu. ... Nimewaambia mambo haya ili furaha yangu iwe ndani yenu na furaha yenu iwe kamili. Amri yangu ndiyo hii: Mpendane kama mimi nilivyowapenda ninyi. Hakuna mtu mwenye upendo mkuu kuliko huu, mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake. Ninyi ni rafiki zangu mkifanya ninayowaamuru. ... Si ninyi mlionichagua, bali mimi ndiye niliyewachagua ninyi na kuwaweka mwende mkazae matunda, na matunda yenu yapate kudumu. Ili nalo lolote mtakalomwomba Baba katika Jina langu, awape ninyi.

*Spiritual Warfare Cards.com*

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yohana 11:25-26, 40-43 (NENO)*

# Yeyote aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele... Je, unasadiki haya?

Yesu akamwambia, "Mimi ndiye huo ufufuo na uzima. Yeye aniaminiye mimi, hata akifa atakuwa anaishi na yeyote aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele. Je, unasadiki haya?" ... Yesu akamwambia, "Sikukuambia kwamba kama ukiamini utauona utukufu wa Mungu?" Kwa hiyo wakaliondoa lile jiwe kutoka kaburini. Yesu akainua macho yake juu akasema, "Baba, ninakushukuru kwa kuwa wanisikia. Ninajua ya kuwa wewe hunisikia siku zote, lakini nimesema haya kwa ajili ya umati huu uliosimama hapa, ili wapate kuamini ya kuwa wewe umenituma." Baada ya kusema haya, Yesu akapaza sauti yake akaita, "Lazaro, njoo huku!"

*Spiritual Warfare Cards.com*

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yohana 12:23-26 (NENO)*

# Mtu yeyote anayependa maisha yake atayapoteza... Mtu yeyote akinitumikia lazima anifuate



Yesu akawajibu, “Saa imewadia ya Mwana wa Adamu kutukuzwa. Amin, amin nawaambia, mbegu ya ngano isipoanguka ardhini na kufa, hubakia kama mbegu peke yake. Lakini ikifa huzaa mbegu nyingi. Mtu yeyote anayependa maisha yake atayapoteza, naye ayachukiaye maisha yake katika ulimwengu huu atayaokoa hata kwa uzima wa milele. Mtu yeyote akinitumikia lazima anifuate, nami mahali nilipo ndipo mtumishi wangu atakapokuwa. Mtu akinitumikia, Baba yangu atamheshimu.



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yohana 14:15, 18-19, 21; 10:27-30 (NENO)*

# Sitawaacha ninyi yatima… kwa kuwa mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai… Kondoo wangu huisikia sauti yangu

---

“Kama mnanipenda, mtazishika amri zangu. … Sitawaacha ninyi yatima, naja kwenu. Bado kitambo kidogo ulimwengu hautaniona tena, ila ninyi mtaniona, kwa kuwa mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai. … Yeyote mwenye amri zangu na kuzishika ndiye anipendaye, naye anipendaye atapendwa na Baba yangu, nami nitampenda na kujidhihirisha kwake.” … Kondoo wangu huisikia sauti yangu nami nawajua, nao hunifuata, nami ninawapa uzima wa milele, hawataangamia kamwe wala hakuna mtu atakayewapokonya kutoka mikono yangu. Baba yangu aliyenipa hawa ni mkuu kuliko wote na hakuna awezaye kuwapokonya kutoka mikononi mwake. Mimi na Baba yangu tu umoja.”



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yohana 16:22, 27, 31-33 (NENO)*

# Ulimwenguni mtapata dhiki. Lakini jipeni moyo, kwa maana mimi nimeushinda ulimwengu



**Hivyo ninyi mna maumivu sasa, lakini nitawaona tena, nayo mioyo yenu itafurahi na furaha yenu hakuna awaondoleaye. … kwa maana Baba mwenyewe anawapenda, kwa sababu mmenipenda mimi na mmeamini kwamba nimetoka kwa Mungu. … Yesu akawajibu, “Je, sasa mnaamini? Saa inakuja, naam, imekwisha kuwadia, mtakapotawanyika kila mmoja kwenda nyumbani kwake na kuniacha peke yangu. Lakini mimi siko peke yangu kwa sababu Baba yu pamoja nami. Nimewaambia mambo haya, ili mpate kuwa na amani mkiwa ndani yangu. Ulimwenguni mtapata dhiki. Lakini jipeni moyo, kwa maana mimi nimeushinda ulimwengu.”**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yohana 17:17-21, 26 (NENO)*

# Uwatakase kwa ile kweli, neno lako ndilo kweli… upendo ule unaonipenda mimi uwe ndani yao na mimi mwenyewe nipate kuwa ndani yao



Uwatakase kwa ile kweli, neno lako ndilo kweli. Kama vile ulivyonituma mimi ulimwenguni, nami nawatuma vivyo hivyo. Kwa ajili yao najiweka wakfu ili wao nao wapate kutakaswa katika ile kweli. “Siwaombei hawa peke yao, bali nawaombea na wale wote watakaoniamini kupitia neno lao ili wawe na umoja kama vile wewe Baba ulivyo ndani yangu na mimi nilivyo ndani yako, wao nao wawe ndani yetu, ili ulimwengu upate kuamini ya kuwa wewe ndiye uliyenituma mimi. … Nimefanya jina lako lijulikane kwao nami nitaendelea kufanya lijulikane, ili kwamba upendo ule unaonipenda mimi uwe ndani yao na mimi mwenyewe nipate kuwa ndani yao.”

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Marko 4:38-40 (NENO)*

# Kwa nini mnaogopa hivyo? Je, bado hamna imani?

---

**Yesu alikuwa katika shetri, akiwa analala juu ya mto. Wanafunzi wake wakamwamsha, wakamwambia, "Mwalimu, hujali kama tunazama?" Akaamka, akaukemea ule upepo, akayaambia yale mawimbi, "Uwe kimya! Tulia!" Ule upepo ukatulia, kukawa shwari kabisa. Yesu akawaambia wanafunzi wake, "Kwa nini mnaogopa hivyo? Je, bado hamna imani?"**



***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Marko 14:36, 38, 61-62 (NENO)*

# Kesheni na mwombe, msije mkaingia majaribuni... Roho iko radhi, lakini mwili ni mdhaifu



Akasema, “Abba, Baba, mambo yote yawezekana kwako. Niondolee kikombe hiki. Lakini si kama nipendavyo mimi, bali vile upendavyo wewe.” ... Kesheni na mwombe, msije mkaingia majaribuni. Roho iko radhi, lakini mwili ni mdhaifu.” ... Lakini Yesu akakaa kimya, hakusema neno lolote. Kuhani mkuu akamuuliza tena, “Je, wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu Aliyebarikiwa?” Yesu akajibu, “Mimi ndimi. Nanyi mtamwona Mwana wa Adamu akiwa ameketi mkono wa kuume wa Mwenye Nguvu, na akija juu ya mawingu ya mbinguni.”

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*1 Wakorintho 10:6, 8, 13 (NENO)*

# Mungu ni mwaminifu; hataruhusu mjaribiwe kupita mnavyoweza



**Basi mambo haya yalitokea kama mifano ili kutuzuia tusiweke mioyo yetu katika mambo maovu kama wao walivyofanya. … Wala tusifanye uzinzi kama baadhi yao walivyofanya, wakafa watu 23,000 kwa siku moja. … Hakuna jaribu lolote lililowapata ambalo si la kawaida kwa wanadamu. Naye Mungu ni mwaminifu; hataruhusu mjaribiwe kupita mnavyoweza. Lakini mnapojaribiwa atawapa njia ya kutokea ili mweze kustahimili.**

*Spiritual Warfare Cards.com*

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*1 Wakorintho 3:1, 3, 16-17 (NENO)*

# Bado kuna wivu na magombano miongoni mwenu... hamjui ya kwamba ninyi wenyewe ni hekalu la Mungu na kwamba Roho wa Mungu anakaa ndani yenu?... hekalu la Mungu ni takatifu



Ndugu zangu, mimi sikuweza kusema nanyi kama watu wa kiroho, bali kama watu wa mwilini, kama watoto wachanga katika Kristo. ... Ninyi bado ni watu wa mwilini. Kwa kuwa bado kuna wivu na magombano miongoni mwenu, je, ninyi si watu wa mwilini? Je, si mwaendelea kama watu wa kawaida? ... Je, hamjui ya kwamba ninyi wenyewe ni hekalu la Mungu na kwamba Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? Kama mtu yeyote akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamwangamiza; kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, na ninyi ndiyo hilo hekalu.



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*1 Wakorintho 6:9-13 (NENO)*

# Mlioshwa, mlitakaswa, mlihesabiwa haki kwa jina la Bwana Yesu Kristo



**Je, hamjui kwamba wasio haki hawataurithi Ufalme wa Mungu? Msidanganyike: Waasherati, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wahanithi, wala walawiti, wala wezi, wala wenye tamaa mbaya, wala walevi, wala wanaodhihaki, wala wanyang'anyi hawataurithi Ufalme wa Mungu. Baadhi yenu mlikuwa kama hao. Lakini mlioshwa, mlitakaswa, mlihesabiwa haki kwa jina la Bwana Yesu Kristo na katika Roho wa Mungu wetu. "Vitu vyote ni halali kwangu": lakini si vitu vyote vyenye faida. "Vitu vyote ni halali kwangu": lakini sitatawaliwa na kitu chochote. "Chakula ni cha tumbo, na tumbo ni la chakula": lakini Mungu ataviangamiza vyote viwili. Mwili haukuumbwa kwa ajili ya zinaa bali kwa ajili ya Bwana na Bwana kwa ajili ya mwili.**



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*2 Wakorintho 1:3-4, 8-9 (NENO)*

# Ahimidiwe Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa huruma na Mungu wa faraja yote... Yeye hutufariji katika taabu zetu

---

**Ahimidiwe Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa huruma na Mungu wa faraja yote. Yeye hutufariji katika taabu zetu, ili tuweze kuwafariji walio katika taabu yoyote kwa faraja ambayo sisi wenyewe tumepokea kutoka kwa Mungu. ... Ndugu wapendwa, hatutaki mkose kujua kuhusu zile taabu tulizopata huko Asia. Kwa maana tulilemewa na mizigo sana, kiasi cha kushindwa kuvumilia, hata tulikata tamaa ya kuishi. Kwa kweli, mioyoni mwetu tulihisi tumekabiliwa na hukumu ya kifo, ili tusijitegemee sisi wenyewe bali tumtegemee Mungu afufuaye wafu.**

*Spiritual Warfare Cards.com*

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*



*2 Wakorintho 4:6-7; 1:12 (NENO)*

# Ameifanya nuru yake ing'ae mioyoni mwetu... tunayo hazina hii katika vyombo vya udongo, ili ijulikane wazi kwamba uwezo huu wa ajabu unatoka kwa Mungu wala si kwetu

Kwa kuwa Mungu, yeye aliyesema, "Nuru na ing'ae gizani," ameifanya nuru yake ing'ae mioyoni mwetu ili kutupatia nuru ya maarifa ya utukufu wa Mungu katika uso wa Kristo. Lakini tunayo hazina hii katika vyombo vya udongo, ili ijulikane wazi kwamba uwezo huu wa ajabu unatoka kwa Mungu wala si kwetu. ... Basi haya ndiyo majivuno yetu: Dhamiri yetu inatushuhudia kwamba tumeenenda katika ulimwengu na hasa katika uhusiano wetu na ninyi, katika utakatifu na uaminifu utokao kwa Mungu. Hatukufanya hivyo kwa hekima ya kidunia bali kwa neema ya Mungu.



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Wagalatia 2:18-21 (NENO)*

# Nimesulubiwa pamoja na Kristo... ninaishi kwa imani ya Mwana wa Mungu, aliyenipenda na kujitoa kwa ajili yangu




Lakini ikiwa mimi ninajenga tena kile ambacho nimekwisha kukibomoa, basi ninaonyesha kwamba mimi ni mkosaji. Kwa maana mimi kwa njia ya sheria, nimeifia sheria ili nipate kuishi kwa ajili ya Mungu. Nimesulubiwa pamoja na Kristo, wala si mimi tena ninayeishi, bali Kristo ndiye aishiye ndani yangu. Uhai nilio nao sasa katika mwili, ninaishi kwa imani ya Mwana wa Mungu, aliyenipenda na kujitoa kwa ajili yangu. Siibatilishi neema ya Mungu, kwa maana kama haki ingeweza kupatikana kwa njia ya sheria, basi Kristo alikufa bure!”

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Wagalatia 6:1-2, 7-9 (NENO)*

# Chukulianeni mizigo ninyi kwa ninyi... Mungu hadhihakiwi... kile apandacho mtu ndicho atakachovuna



**Ndugu zangu, ikiwa mtu ameghafilika akatenda dhambi, basi ninyi mlio wa rohoni, mrejesheni upya mtu huyo kwa roho ya upole. Lakini jihadharini, ili ninyi wenyewe msije mkajaribiwa. Chukulianeni mizigo ninyi kwa ninyi, nanyi kwa njia hii mtatimiza sheria ya Kristo. ... Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi. Kwa kuwa kile apandacho mtu ndicho atakachovuna. Apandaye kwa mwili, katika mwili wake atavuna uharibifu, lakini yeye apandaye katika Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele. Hivyo, tusichoke katika kutenda mema, kwa kuwa tutavuna kwa wakati wake tusipokata tamaa.**

*Spiritual Warfare Cards.com*

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*1 Timotheo 4:6-8, 10 (NENO)*

# Jizoeze kuwa mtauwa... tumeweka tumaini letu kwa Mungu aliye hai

Kama ukiwakumbusha ndugu mambo haya, utakuwa mtumishi mwema wa Kristo Yesu, uliyelelewa katika kweli ya imani na yale mafundisho mazuri uliyoyafuata. Usijishughulishe kamwe na hadithi za kipagani na masimulizi ya uongo ya wanawake wazee; badala yake, jizoeze kuwa mtauwa. Kwa maana mazoezi ya mwili yana faida kwa sehemu, lakini utauwa una faida katika mambo yote, yaani, unayo ahadi ya uzima wa sasa na ya ule ujao. ... (nasi kwa ajili ya hili tunajitaabisha na kujitahidi), kwamba tumeweka tumaini letu kwa Mungu aliye hai, ambaye ni Mwokozi wa watu wote, hasa wale waaminio.

*Spiritual Warfare Cards.com*

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*1 Timotheo 6:11-16 (NENO)*

# Pigana vile vita vizuri vya imani. Shika uzima wa milele... uishike amri hii bila dosari wala lawama

---

**Lakini wewe, mtu wa Mungu, yakimbie mambo haya yote. Fuata haki, utauwa, imani, upendo, saburi na upole. Pigana vile vita vizuri vya imani. Shika uzima wa milele ambao ndio ulioitiwa ulipokiri ule ukiri mzuri mbele ya mashahidi wengi. Nakuagiza mbele za Mungu avipaye vitu vyote uhai, na mbele za Kristo Yesu ambaye alipokuwa anashuhudia mbele ya Pontio Pilato alikiri ukiri mzuri, uishike amri hii bila dosari wala lawama mpaka kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye Mungu atamleta kwa wakati wake mwenyewe: yeye ahimidiwaye, aliye peke yake Mtawala, Mfalme wa wafalme, na Bwana wa mabwana, yeye peke yake ambaye hapatikani na mauti, na anakaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa, ambaye hakuna mwanadamu aliyemwona wala awezaye kumwona. Heshima na uweza una yeye milele. Amen.**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*2 Timotheo 1:6-8, 12 (NENO)*

# Mungu hakutupa roho ya woga, bali roho ya nguvu, ya upendo na ya moyo wa kiasi



Kwa sababu hii nakukumbusha uchochee ile karama ya Mungu, iliyowekwa ndani yako nilipokuwekea mikono yangu. Maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali roho ya nguvu, ya upendo na ya moyo wa kiasi. Kwa hiyo usione haya kushuhudia kuhusu Bwana wetu, wala usinionee haya mimi niliye mfungwa kwa ajili yake. Bali uishiriki pamoja nami taabu ya Injili, kwa kadiri ya nguvu ya Mungu, … Hii ndiyo sababu ninateseka namna hii, lakini sioni haya kwa maana ninamjua yeye niliyemwamini, na kusadiki ya kuwa anaweza kukilinda kile nilichokiweka amana kwake hadi siku ile.

*Spiritual Warfare Cards.com*

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*1 Timotheo 1:3-5; 6:20-21 (NENO)*

# Linda kile kilichowekwa amana kwako... Epuka majadiliano yasiyo ya utauwa

---

**Kama nilivyokusihi wakati nilipokwenda Makedonia, endelea kubaki Efeso, ili kwamba upate kuwaagiza watu wasiendelee kufundisha mafundisho ya uongo wala wasitoe muda wao kwa hadithi za kubuniwa na orodha za majina ya vizazi visivyo na mwisho, ambazo huchochea mabishano badala ya mpango wa Mungu utokanao na imani. Kusudi la maagizo haya ni upendo utokao katika moyo safi, dhamiri njema na imani ya kweli. ... Timotheo, linda kile kilichowekwa amana kwako. Epuka majadiliano yasiyo ya utauwa na mabishano ambayo kwa uongo huitwa elimu, ambayo wengine kwa kujidai kuwa nayo wameiacha imani. Neema iwe nanyi. Amen.**

*Spiritual Warfare Cards.com*

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yakobo 1:1-5 (NENO)*

# Kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi... Kama mtu yeyote miongoni mwenu amepungukiwa na hekima na amwombe Mungu

**Yakobo, mtumwa wa Mungu na wa Bwana Yesu Kristo: Kwa makabila kumi na mawili yaliyotawanyika ulimwenguni: Salamu. Ndugu zangu, hesabuni kuwa ni furaha tupu mnapopatwa na majaribu mbalimbali, kwa sababu mnajua ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi. Saburi na iwe na kazi timilifu, ili mpate kuwa wakamilifu, mmekamilishwa, bila kupungukiwa na kitu chochote. Kama mtu yeyote miongoni mwenu amepungukiwa na hekima na amwombe Mungu, yeye awapaye watu wote kwa ukarimu wala hana kinyongo, naye atapewa.**





*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yakobo 5:13-14, 16, 19-20 (NENO)*

# Ungamianeni dhambi zenu ninyi kwa ninyi na kuombeana... ataiokoa roho ya huyo mwenye dhambi kutoka mauti



Je, mtu yeyote miongoni mwenu amepatwa na taabu? Basi inampasa aombe. Je, kuna yeyote mwenye furaha? Basi na aimbe nyimbo za kusifu. Je, kuna yeyote miongoni mwenu aliye mgonjwa? Basi inampasa awaite wazee wa kanisa wamwombee na kumpaka mafuta kwa Jina la Bwana. ... Kwa hiyo ungamianeni dhambi zenu ninyi kwa ninyi na kuombeana ili mpate kuponywa. Maombi ya mwenye haki yana nguvu tena yanafaa sana. ... Ndugu zangu, yeyote miongoni mwenu akipotoka na kuicha kweli, naye akarejezwa na mtu mwingine, hamna budi kujua kwamba yeyote amrejezaye mwenye dhambi kutoka upotovu wake, ataiokoa roho ya huyo mwenye dhambi kutoka mauti na kusitiri wingi wa dhambi.

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yakobo 3:2, 10, 12, 18, 17 (NENO)*

# Sisi sote tunajikwaa katika mambo mengi… hekima itokayo mbinguni kwanza ni safi, kisha inapenda amani, tena ni ya upole… isiyopendelea mtu, tena isiyokuwa na unafiki

---

Sisi sote tunajikwaa katika mambo mengi. Ikiwa mtu yeyote hakosei kamwe katika yale anayosema, yeye ni mkamilifu, naye anaweza kuuzuia pia na mwili wake wote. … Katika kinywa kile kile hutoka baraka na laana. Ndugu zangu, haistahili kuwa hivyo. … Je, ndugu zangu, mtini waweza kuzaa zeituni, au mzabibu kuzaa tini? Wala chemchemi ya maji ya chumvi haiwezi kutoa maji matamu. … Mavuno ya haki hupandwa katika amani na wale wafanyao amani. … Lakini hekima itokayo mbinguni kwanza ni safi, kisha inapenda amani, tena ni ya upole, iliyo tayari kusikiliza wengine kwa unyenyekevu, iliyojaa huruma na matunda mema, isiyopendelea mtu, tena isiyokuwa na unafiki.

*Spiritual Warfare Cards.com*

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yuda 1:3-5, 22-23 (NENO)*

# Mwitetee imani iliyokabidhiwa watakatifu kwa nafasi moja itoshayo... wapotoshao neema ya Mungu wetu kuwa ufisadi

Wapendwa, ingawa nilikuwa ninatamani sana kuwaandikia kuhusu wokovu ambao tunaushiriki sisi sote, niliona imenipasa kuwaandikia na kuwasihi kwamba mwitetee imani iliyokabidhiwa watakatifu kwa nafasi moja itoshayo. Kwa kuwa kuna watu waliojipenyeza kwa siri katikati yenu, watu walioandikiwa tangu zamani hukumu hii, waovu, wapotoshao neema ya Mungu wetu kuwa ufisadi wakimkana yeye aliye Bwana wetu wa pekee, Bwana Yesu Kristo. Ingawa mmekwisha kujua haya yote, nataka niwakumbushe kuwa Bwana akiisha kuwaokoa watu wake kutoka nchi ya Misri, baadaye aliwaangamiza wale ambao hawakuamini. ... Wahurumieni walio na mashaka; wengine waokoeni kwa kuwanyakua kutoka kwenye moto; nao wengine wahurumieni mkiwa na hofu, mkichukia hata vazi lenye mawaa na kutiwa unajisi na mwili.



*Spiritual Warfare Cards.com*

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Kutoka 24:7, 17; 32:23, 30, 34 (NENO)*

# Utukufu wa Bwana ulionekana kama moto uteketezao juu ya mlima



Kisha akachukua kile Kitabu cha Agano na kuwasomea watu. Nao wakajibu, “Tutafanya kila kitu alichosema Bwana, nasi tutatii.” … Kwa Waisraeli utukufu wa Bwana ulionekana kama moto uteketezao juu ya mlima. … Wao waliniambia, ‘Tufanyie miungu itakayotuongoza. Kwa kuwa huyu jamaa yetu Mose aliyetupandisha kutoka Misri, hatufahamu yaliyompata.’ … Siku iliyofuata Mose akawaambia watu, “Mmefanya dhambi kubwa. Lakini sasa nitapanda juu kwa Bwana, labda nitaweza kufanya upatanisho kwa ajili ya dhambi yenu.” … Sasa nenda, uongoze hao watu mpaka mahali nilipokuambia, naye malaika wangu atakutangulia. Pamoja na hayo, wakati utakapofika wa mimi kuwaadhibu, nitawaadhibu kwa ajili ya dhambi yao.”

*Spiritual Warfare Cards.com*

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yoshua 2:11; Waebrania 11:31; Yakobo 2:23, 25-26 (NENO)*

# Bwana Mungu wenu ni Mungu juu mbinguni na duniani chini... imani pasipo matendo imekufa



**Tuliposikia juu ya hili, mioyo yetu iliyeyuka na kila mmoja alikosa ujasiri kwa sababu yenu, kwa maana Bwana Mungu wenu ni Mungu juu mbinguni na duniani chini. ... Kwa imani, Rahabu, yule kahaba, hakuangamizwa pamoja na wale waliomwasi Mungu, kwa kuwa aliwakaribisha wale wapelelezi. ... Kwa njia hiyo yakatimizwa yale Maandiko yasemayo, “Abrahamu alimwamini Mungu na ikahesabiwa kwake kuwa haki,” naye akaitwa rafiki wa Mungu. ... Vivyo hivyo, hata Rahabu, yule kahaba, hakuhesabiwa haki kwa yale aliyotenda alipowapokea wale wapelelezi na kuwaambia waende njia nyingine? Kama vile ambavyo mwili pasipo roho umekufa, kadhalika nayo imani pasipo matendo imekufa.**

*Spiritual Warfare Cards.com*

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Ruthu 1:16-17; 4:14-15 (NENO)*

# Ahimidiwe Bwana, asiyekuacha bila kuwa na jamaa wa karibu wa kukomboa



**Lakini Ruthu akajibu, “Usinisihi nikuache au niache kukufuata. Utakakokwenda nami nitakwenda, na wewe utakapoishi nitaishi. Watu wako watakuwa watu wangu, na Mungu wako atakuwa Mungu wangu. Pale utakapofia nami nitafia hapo, na papo hapo nitazikwa. Bwana na aniadhibu vikali, kama kitu kingine chochote kitanitenga nawe isipokuwa kifo.” … Wanawake wakamwambia Naomi: “Ahimidiwe Bwana, asiyekuacha bila kuwa na jamaa wa karibu wa kukomboa. Na awe mashuhuri katika Israeli yote! Atakurejeshea uhai wako na kukuangalia katika siku za uzee wako. Kwa maana mkweo ambaye anakupenda, na ambaye kwako ni bora zaidi ya watoto wa kiume saba, ndiye alimzaa.”**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Nehemia 6:1-3, 8-9 (NENO)*

# Wote walikuwa wakijaribu kutuogopesha… Ee Mungu, sasa nitie mikono yangu nguvu



**Habari zilipofika kwa Sanbalati, Tobia, Geshemu Mwarabu, na adui zetu wengine kwamba nimejenga tena ukuta na hakuna nafasi iliyobakia ndani mwake, ingawa mpaka wakati huo sikuwa nimeweka milango kwenye malango, Sanbalati na Geshemu wakanitumia ujumbe huu: "Njoo, tukutane katika mojawapo ya vijiji katika nchi tambarare ya Ono." Lakini walikuwa wakikusudia kunidhuru. Kwa hiyo niliwatuma wajumbe kwao na majibu haya: "Kazi ninayoifanya ni kubwa sana, siwezi kuja. Kwa nini niiache kazi isimame nije kwenu?" … Nilimpelekea jibu hili: "Hakuna jambo kama hilo unalosema linalofanyika. Unalitunga tu kwenye kichwa chako." Wote walikuwa wakijaribu kutuogopesha, wakifikiri hivi: "Mikono ya watu italegea kiasi kwamba hawataweza kufanya kazi, nayo haitakamilika." Lakini niliomba, "Ee Mungu, sasa nitie mikono yangu nguvu."**



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Zaburi 2:1-5, 8-12 (NENO)*

# Mtumikieni Bwana kwa hofu... Heri wote wanaomkimbilia

**Kwa nini mataifa wanashauriana kufanya mabaya, na kabila za watu kula njama bure? Wafalme wa dunia wanajipanga na watawala wanajikusanya pamoja dhidi ya Bwana na dhidi ya Mpakwa Mafuta wake. Wanasema, "Tuvunje minyororo yao na kuvitupilia mbali vifungo vyao." Yeye atawalaye mbinguni hucheka, Bwana huwadharau. Kisha huwakemea katika hasira yake na kuwaogopesha katika ghadhabu yake, akisema, ... Niombe, nami nitayafanya mataifa kuwa urithi wako, miisho ya dunia kuwa milki yako. Utawatawala kwa fimbo ya chuma na kuwavunjavunja kama chombo cha mfinyanzi." Kwa hiyo, ninyi wafalme, kuweni na hekima; mwonyeke, enyi watawala wa dunia. Mtumikieni Bwana kwa hofu na mshangilie kwa kutetemeka. Mbusu Mwana, asije akakasirika nawe ukaangamizwa katika njia yako, kwa maana hasira yake inaweza kuwaka ghafula. Heri wote wanaomkimbilia.**



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Zaburi 19:1, 7-8, 12-14 (NENO)*

# Mbingu zinatangaza utukufu wa Mungu... Nisamehe makosa yangu nisiyoyajua... Mlinde mtumishi wako na dhambi za makusudi, nazo zisinitawale

---

Mbingu zinatangaza utukufu wa Mungu, anga zahubiri kazi ya mikono yake. ... Sheria ya Bwana ni kamilifu, ikihuisha nafsi. Shuhuda za Bwana ni za kuaminika, zikimpa mjinga hekima. Maagizo ya Bwana ni kamili, nayo hufurahisha moyo. Amri za Bwana huangaza, zatia nuru machoni. ... Ni nani awezaye kutambua makosa yake? Nisamehe makosa yangu nisiyoyajua. Mlinde mtumishi wako na dhambi za makusudi, nazo zisinitawale. Ndipo nitakapokuwa sina lawama, wala sitakuwa na hatia ya kosa kubwa. Maneno ya kinywa changu na mawazo ya moyo wangu, yapate kibali mbele zako, Ee Bwana, Mwamba wangu na Mkombozi wangu.

*Spiritual Warfare Cards.com*

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Zaburi 27:1, 4-6, 8-10, 14 (NENO)*

# Bwana ni nuru yangu na wokovu wangu, nimwogope nani?... uwe hodari na mwenye moyo mkuu

---

Bwana ni nuru yangu na wokovu wangu, nimwogope nani? Bwana ni ngome ya uzima wangu, nimhofu nani? ... Jambo moja ninamwomba Bwana, hili ndilo ninalolitafuta: niweze kukaa nyumbani mwa Bwana siku zote za maisha yangu, niutazame uzuri wa Bwana na kumtafuta hekaluni mwake. Kwa kuwa siku ya shida, atanihifadhi salama katika maskani yake, atanificha uvulini mwa hema yake na kuniweka juu kwenye mwamba. Kisha kichwa changu kitainuliwa juu ya adui zangu wanaonizunguka. Katika maskani yake nitatoa dhabihu kwa kelele za shangwe; nitamwimbia Bwana na kumsifu. ... Moyo wangu unasema kuhusu wewe, “Utafute uso wake!” Uso wako, Bwana “Nitautafuta.” Usinifiche uso wako, usimkatae mtumishi wako kwa hasira; wewe umekuwa msaada wangu. Usinikatae wala usiniache, Ee Mungu Mwokozi wangu. Hata kama baba yangu na mama wakiniacha, Bwana atanipokea. ... Mngojee Bwana, uwe hodari na mwenye moyo mkuu, nawe, umngojee Bwana.

*Spiritual Warfare Cards.com*

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Zaburi 29:2-3, 7-11 (NENO)*

# Mungu wa utukufu hupiga radi... Bwana huwapa watu wake nguvu; Bwana huwabariki watu wake kwa kuwapa amani



Mpeni Bwana utukufu unaostahili jina lake; mwabuduni Bwana katika uzuri wa utakatifu wake. Sauti ya Bwana iko juu ya maji; Mungu wa utukufu hupiga radi, Bwana hupiga radi juu ya maji makuu. ... Sauti ya Bwana hupiga kwa miali ya umeme wa radi. Sauti ya Bwana hutikisa jangwa; Bwana hutikisa Jangwa la Kadeshi. Sauti ya Bwana huzalisha ayala, na huuacha msitu wazi. Hekaluni mwake wote wasema, “Utukufu!” Bwana huketi akiwa ametawazwa juu ya gharika; Bwana ametawazwa kuwa Mfalme milele. Bwana huwapa watu wake nguvu; Bwana huwabariki watu wake kwa kuwapa amani.

*Spiritual Warfare Cards.com*

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Marko 9:23-26, 29; 1:27 (NENO)*

# Ninaamini. Nisaidie kutokuamini kwangu!... Hali hii haiwezi kutoka isipokuwa kwa kuomba na kufunga

Yesu akamwambia, “Kama ukiweza kuamini, yote yawezekana kwake yeye aaminiye.” Mara baba yake yule mvulana akapiga kelele akisema, “Ninaamini. Nisaidie kutokuamini kwangu!” Yesu alipoona kwamba umati wa watu unakusanyika pamoja mbio, akamkemea yule pepo mchafu, akimwambia, “Wewe pepo bubu na kiziwi, nakuamuru umtoke, wala usimwingie tena!” Yule pepo mchafu akiisha kupiga kelele, akamtia kifafa kwa nguvu, na akamtoka. ... Yesu akawajibu, “Hali hii haiwezi kutoka isipokuwa kwa kuomba na kufunga.” ... Watu wote wakashangaa, hata wakaulizana wao kwa wao, “Haya ni mambo gani? Ni mafundisho mapya, tena yenye mamlaka! Anaamuru hata pepo wachafu, nao wanamtii!”



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Zaburi 22:1, 16-18, 26, 29, 31 (NENO)*

# Wale wamtafutao Bwana watamsifu: mioyo yenu na iishi milele!



**Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha? Kwa nini uko mbali hivyo kuniokoa? Mbali hivyo na maneno ya kuugua kwangu? … Mbwa wamenizunguka, kundi la watu waovu limenizingira, wametoboa mikono yangu na miguu yangu. Naweza kuhesabu mifupa yangu yote, watu wananikodolea macho na kunisimanga. Wanagawana nguo zangu wao kwa wao, na vazi langu wanalipigia kura. … Maskini watakula na kushiba, wale wamtafutao Bwana watamsifu: mioyo yenu na iishi milele! … Matajiri wote wa dunia watasherehekea na kuabudu. Wote waendao mavumbini watapiga magoti mbele yake, wote ambao hawawezi kudumisha uhai wao. … Watatangaza haki yake kwa watu ambao hawajazaliwa bado, kwa maana yeye ametenda hili.**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Wimbo Ulio Bora 8:6-7; 2:15-16 (NENO)*

# Nitie kama muhuri moyoni mwako... upendo una nguvu kama mauti... wivu wake ni mkatili kama kuzimu



---

**Nitie kama muhuri moyoni mwako, kama muhuri kwenye mkono wako; kwa maana upendo una nguvu kama mauti, wivu wake ni mkatili kama kuzimu. Unachoma kama mwali wa moto, kama mwali mkubwa wa moto wa Bwana hasa. Maji mengi hayawezi kuuzimisha upendo, mito haiwezi kuugharikisha. Kama mtu angelitoa mali yote ya nyumbani mwake kwa ajili ya upendo, angelidharauliwa kabisa. ... Tukamatie mbweha, mbweha wale wadogo wanaoharibu mashamba ya mizabibu, mashamba yetu ya mizabibu yaliyochanua. Mpenzi wangu ni wangu, nami ni wake, yeye hujilisha katikati ya yungiyungi.**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Maombolezo 3:22-23, 25-26, 28-29, 32 (NENO)*

# Bwana ni mwema kwa wale ambao tumaini lao ni kwake, kwa yule ambaye humtafuta

---

**Kwa sababu ya upendo mkuu wa Bwana, hatuangamii, kwa kuwa huruma zake hazikomi kamwe. Ni mpya kila asubuhi, uaminifu wako ni mkuu. … Bwana ni mwema kwa wale ambao tumaini lao ni kwake, kwa yule ambaye humtafuta; ni vyema kungojea kwa utulivu kwa ajili ya wokovu wa Bwana. … Na akae peke yake awe kimya, kwa maana Bwana ameiweka juu yake. Na azike uso wake mavumbini bado panawezekana kuwa na matumaini. … Ingawa huleta huzuni, ataonyesha huruma, kwa kuwa upendo wake usiokoma ni mkuu.**



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Hosea 2:2, 13, 8, 14, 19-20; 6:6 (NENO)*

# Aondoe sura ya uzinzi katika uso wake... nawe utamkubali Bwana... nataka rehema, wala si dhabihu

"Mkemeeni mama yenu, mkemeeni, kwa maana yeye si mke wangu, nami si mume wake. Aondoe sura ya uzinzi katika uso wake na uzinzi kati ya matiti yake. ... Nitamwadhibu kwa ajili ya siku alizowafukizia uvumba Mabaali; alipojipamba kwa pete na kwa vito vya thamani, na kuwaendea wapenzi wake, lakini mimi alinisahau," asema Bwana. ... Gomeri hajakubali kuwa mimi ndiye niliyempa nafaka, divai mpya na mafuta, niliyemwongezea fedha na dhahabu waliyoitumia kwa kumtumikia Baali. ... "Kwa hiyo sasa nitamshawishi; nitamwongoza hadi jangwani na kuzungumza naye kwa upole. ... Nitakuposa uwe wangu milele; nitakuposa kwa uadilifu na haki, kwa upendo na huruma. Nitakuposa kwa uaminifu, nawe utamkubali Bwana. ... Kwa maana nataka rehema, wala si dhabihu, kumkubali Mungu zaidi kuliko sadaka za kuteketezwa.



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Amosi 5:21-24 (NENO)*

# Acheni haki itiririke kama mto, na uadilifu uwe kama kijito kisichokauka

---

**"Ninachukia, ninazidharau sikukuu zenu za dini; siwezi kuvumilia makusanyiko yenu. Hata ingawa mnaniletea sadaka zenu za kuteketezwa na sadaka za nafaka, sitazikubali. Ingawa mnaniletea sadaka nzuri za amani, sitazitambua. Niondoleeni kelele za nyimbo zenu! Sitasikiliza sauti za vinubi vyenu. Lakini acheni haki itiririke kama mto, na uadilifu uwe kama kijito kisichokauka!**



***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Sefania 1:14-15; 3:17 (NENO)*

# Siku ya uharibifu na ukiwa... yeye ni mwenye nguvu kuokoa... atakufurahia kwa kuimba



**“Siku kubwa ya Bwana iko karibu: iko karibu na inakuja haraka. Sikilizeni! Kilio katika siku ya Bwana kitakuwa kichungu, hata shujaa atapiga kelele. Siku ile ni siku ya ghadhabu, siku ya fadhaa na dhiki, siku ya uharibifu na ukiwa, siku ya giza na utusitusi, siku ya mawingu na giza nene, ... Bwana Mungu wako yu pamoja nawe, yeye ni mwenye nguvu kuokoa. Atakufurahia kwa furaha kubwa, atakutuliza kwa pendo lake, atakufurahia kwa kuimba.”**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Habakuki 3:16-19 (NENO)*

# Ingawa mtini hauchanui maua... hata mashamba hayatoi chakula... nitamfurahia Mungu Mwokozi wangu

---

**Nilisikia na moyo wangu ukagonga kwa nguvu, midomo yangu ikatetemeka kwa hofu niliposikia sauti; uchakavu ukanyemelea mifupa yangu, na miguu yangu ikatetemeka. Hata hivyo nitasubiri kwa uvumilivu siku ya maafa kuyajilia mataifa yaliyotuvamia. Ingawa mtini hauchanui maua na hakuna zabibu juu ya mizabibu, ingawaje mzeituni hauzai, na hata mashamba hayatoi chakula, iwapo hakuna kondoo katika banda, wala ng'ombe katika zizi, hata hivyo nitashangilia katika Bwana, nitamfurahia Mungu Mwokozi wangu. Bwana Mwenyezi ni nguvu yangu; huifanya miguu yangu kama miguu ya ayala, huniwezesha kupita juu ya vilima. Kwa kiongozi wa uimbaji. Kwa vinanda vyangu vya nyuzi.**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*